**UCHANGANUZI WA MITAZAMO YA KIIMANI NA KISEKULA KUHUSU LUGHA**

**(1) Yasin S. Musa, PhD, (2) Badru M. Haroon, PhD (3) Nawaje A. Mganga PhD**

**By**

Dr. Yasin S. Musa is a lecturer in the Department of Literature, Language and Linguistics, Faculty of Arts and Social Sciences, Islamic University in Uganda.

Dr. Matasi Badru Haroon is a former lecturer of Kiswahili in the same Department.

Dr. Nawaje Ali Mganga is a lecturer and head of Kiswahili Department, Muslim University of Morogoro.

**Ikisiri**

*Lugha ni nyenzo ya kipekee katika mawasiliano ya viumbe vyote. Kwa karne nyingi dhana ya lugha imeibua mijadala mingi kiasi cha kuwafanya wanaisimu kubaki njia panda kutokana na kukosa mwafaka kuhusu maana na chanzo cha lugha. Ingawa kuna imani tofauti katika uso wa dunia hii, lakini imani zenye wafuasi wengi ni Ukristo na Uislamu. Kwa mnasaba wa makala hii, mtazamo wa kiimani utakaorejelewa ni imani ya Kiislamu, na hizo imani nyengine zitadokezwa tu itakapobidi. Mathalan, Usekula ni imani isiyojinasibisha na maswala ya kidini katika maendeleo ya jamii kupitia nyanja zote za kimaisha. Wasekula hawaamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, Muumba wa ardhi na mbingu na vyote vilivyomo ndani yake; akiwemo mwanadamu na lugha, bali huamini kuwa vimetokea kwa bahati nasibu tu; na kwa hivyo vitatoweka pasi na utaratibu mahsusi. Ukristo hueleza kuwa lugha ni zawadi kutoka kwa Mungu wa Adamu; ndiye aliyevipa vitu vyote majina. Vivyo hivyo, unashikilia kuwa tofauti ya ndimi chanzo chake ni utengano uliojitokeza baada ya mnara wa Babeli kuanguka na watu waliokuwa wanaupanda kutapakaa sehemu mbalimbali. Uislamu ni dini inayoamini kwamba asili na chanzo cha lugha ni Mwenyezi Mungu. Ni neema ya Mwenyezi Mungu[1] kwa viumbe wake katika mawasiliano ili wapate kulifikia vyema lengo la kuumbwa kwao. Kwa mantiki hiyo, mjadala wa makala hii umeiangalia lugha kwa mtazamo wa Kiislamu kama inavyoelezewa katika mafundisho yake,*

[1] Mwenyezi Mungu anayekusudiwa au anayeaminiwa na Waislamu, ambaye kwa itikadi yao ndiye muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo anaitwa Allah kwa Kiarabu.

**Utangulizi**

Ifahamike kwamba Nadharia ya Kidini husema kwamba lugha ya Adamu (Lingua Adamica) ndiyo ilikuwa lugha ya mwanzo na lugha mbalimbali zilitokana na lugha hiyo moja zikiwa ni lahaja zake. Wanaoshikilia nadharia hii hutumia usifabia (Language Universals) kama ushahidi ambapo wanasema lugha zote hubadilika, zina nomino na maneno mengine yana maana sawa.

Biblia huelezea katika kitabu cha Mwanzo (11:1) kwamba hapo kale dunia yote ilizungumza lugha moja. Mwanzo (2:19) hutaja kwamba Adam alipewa mamlaka ya kuvipa viumbe vyote majina (Crystal, 1989; Fromkin na Rodman, 1993 na Byakutaga, 2000). Ukristo unashikilia kuwa lugha zote zilitokana na lugha moja iliyoumbwa na Mungu na baadaye lugha nyingi zikazuka kutokana na utengano uliojitokeza katika mnara wa Babeli. Inadaiwa kuwa wanadamu walikuwa wakizungumza lugha moja mpaka wakati walipoamua kujenga mnara ili wamfikie Mungu. Kwa vile Mungu hakupendezwa na kitendo hicho alizusha tofauti za kilugha kati yao na ikawapelekea kutoelewana. Matokeo yake yakawa ni kutokuendelea na mradi wa ujenzi wa mnara wa Babeli na hatimaye wakatawanyika. Imani hii ya Kikristo inakutana na kuachana na ile ya Kiislamu; inakutana katika asili ya lugha ni Mwenyezi Mungu lakini inaachana katika kuibuka kwa lugha mbalimbali, hili litafafanuliwa kwa fasili baadaye.

Wahindu huamini kwamba lugha ilitokana na Mungu wa kike Sarasvati ambaye ni mke wa Mungu wao aitwaye Brahama. Maono haya yanakosa fahiwa.

Usekula ni imani ambayo haihusishi maswala ya kidini na maendeleo ya jamii katika nyanja zote za kimaisha. Wasekula hawaamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu muumba wa ardhi na mbingu na vyote vilivyomo ndani yake, wala hawaamini kuwa mwanadamu na vyote vilivyomo vimeumbwa na Mwenyezi Mungu; bali huamini kuwa vimetokea kwa bahati nasibu tu! Wasekula hawaamini kuwa kuna maisha baada ya kufa. Hii ni kutokana na kukana kwao umbile la mwanadamu kuwa limejengwa kwa vitu viwili vikuu: roho na mwili; na wao huamini mwili tu.

Kwa mujibu wa Lado (1964) anasema: “Lugha ni chombo cha kuwasiliana miongoni mwa binadamu wa jamii moja. Lugha kwa upande wake na undani wake inahusiana na kuwasiliana kwa kusema na kusikia. Akitomelea anaendelea kusema, lugha hutumia alama kwa kusema na kusikia, ambazo ni **nasibu** katika kuambatana kwazo na maana maalumu. Naye Nkwera (1979)

anasema: “Lugha ni **mfumo wa sauti za nasibu** zenye kubeba maana na zilizokubaliwa na jamii ya watu zitumike katika kuwasiliana”. Wakadhalika Mhina na Kiimbila, (1971) wanasema, “Lugha ni utaratibu (mfumo) kamili wa sauti za kusemwa, **sauti za nasibu**, za watu wa utamaduni fulani, watumiao kupashana habari”. Unasibu unaosisitizwa na wataalamu hao, huashiria kwamba lugha ilizuka tu na mwanadamu kakutana nayo hapa duniani kwa sadfa. Hii ni kumaanisha yaweza kumtoka mwanadamu kwa fikra hizohizo zao kwamba hata mwanadamu kabahatika kwa bahati nasibu na ndivyo vivyo hivyo naye atatoweka kwa bahati nasibu na kila chake ikiwemo lugha.

Mtazamo huo wa kinasibu ndiwo unaoziafiki nadharia za kianzo asili na ishara; ambapo inadaiwa kwamba maneno tuliyonayo ulimwenguni yalitokana na miigo ya sauti za wanyama. Watu wa kale walioishi mwituni waliiga sauti za wanyama na baadaye wakazitumia katika mawasiliano yao. Baadhi ya sauti hizo zilizoigwa ilisadikiwa kuwa ni kama vile: “cukoo” iliyozaa maneno kama vile: “kuku”, “cock” (Kiingereza), na “Nguku” (Kikikuyu, Kipare na lugha nyinginezo za Kibantu kwa mintaarafu ya mifano hiyo) kutokana na sauti inayotolewa na ndege huyu. Kwa lugha za kileo maneno hayo huitwa *onomatopia*. Wako wengine wakidai kuwa lugha ilitokana na furaha au machungu waliyokumbana nayo watu.

Milio husemekana ndiyo iliyoelekeza kuweko kwa lugha. Wengine walidai kwamba lugha ilitokana na sauti zilizotokana na watu waliokuwa wakifanya kazi kwa pamoja; ambapo walitoa milio fulani iliyolenga kuwashirikisha watu kufanya kazi. Aidha, iliaminiwa kwamba matumizi ya sauti yalitokana na ishara za mwili hususani ulimi na midomo kwa minajili ya mawasiliano. Wasekula wamekosa imani kuhusu kuwepo kwa Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi; ambapo walipaswa kuamini kwamba, mwanadamu na kila chake - chanzo chake ni Mwenyezi Mungu; kama Mwenyezi Mungu alivyotanabaisha kwamba kila kilichomo mbinguni na ardhini (ikiwemo lugha) vimeumbiwa mwanadamu ili aweze kulifikia lengo la kuumbwa kwake.

Ingawa kuna njia mbalimbali za mawasiliano lakini lugha ni nyenzo muhimu katika mawasiliano, kutokana na umuhimu wake ndiyo maana imekuwa katika kurasa za mijadala ya wanaisimu wenye mrengo wa itikadi za kidini na wale wasio na mrengo wa itikadi za kidini. Hata katika misahafu mitakatifu lugha haikufumbiwa macho bali imezungumzwa kwa namna yake. Uislamu ni moja ya imani za kidini iliyohubiriwa na mitume wengi; tangu Adam (A.S) na

kuhitimishwa na Muhammad (S.A.W) katika karne ya saba. Kama Kur'ani isemavyo "...Yeye (Mwenyezi Mungu) alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Kur'ani) pia..." (Kur'ani, 22:78). Inaaminika kuwa Uislamu ni dini iliyojikita katika vipengele vyote vya maisha ya mwanadamu kikiwemo kipengele cha lugha. Kwa hivyo, uchambuzi wa makala hii umemili katika maana, chanzo, sifa za lugha, maelezo yafuatayo yanafafanua.

**Mtazamo wa Uislamu kuhusu Lugha**

**(i) Fasili ya Lugha**

Lugha imefasiliwa kama mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake ili kuwasiliana kati yao (Mgullu, 2012). Fasili hiyo ni ya Kisekula kwani haikutilia maanani suala la dini ambayo wanasayansi huichukulia kuwa hushughulikia mambo ya kidhanifu yasiyo mbali sana na uyakinifu (Mounir na wenzake, 1980). Kwa mtazamo wa Uislamu fikra hizo za kimagharibi katika kuelezea lugha zina udhaifu. Ibin Taimiyya mwanazuoni maarufu wa Kiislamu, ameifasili lugha kama njia ya mawasiliano anayoitumia mwanadamu kuelezea mambo anayoyatambua na kuyahisi. Lugha ni chombo cha mawasiliano ambacho hutegemea mfumo, hisia au akili; na ni ala inayotumika katika upataji wa elimu (Abdussalam, 2006). Kwa mantiki hiyo, lugha ni mfumo bainifu ambao Mwenyezi Mungu amewajaalia wanadamu si tu waweze kuwasiliana baina yao; lakini pia watambue kuwepo kwake, nguvu zake na matakwa yake.

Fasili hiyo hutupilia mbali suala la unasibu linalojitokeza katika mtazamo wa Kisekula. Fauka ya hayo, inaihusisha lugha na Mwenyezi Mungu kama inavyohusisha na kuumbwa kwa mwanadamu. Kwa hivyo, mtazamo wa Kiislamu hukinzana na ule wa Kisekula uliojengwa juu ya msingi wa unasibu ulioasisiwa na Darwin anayeshikilia kuwa mwanadamu aliibuka kwa bahati nasibu ama kwa sadifa tu na siyo vinginevyo (Balta, 2007:16). Ingawa unasibu wa lugha unasemwa kuwa hakuna sababu ya kitu kuitwa kwa jina fulani, hakuna siku jamii ilikubaliana juu ya dhana fulani lakini kwa mtazamo wa Uislamu hakuna unasibu wa aina yoyote kati ya hizo ila Mwenyezi Mungu ndiye muumbaji na mwanzishaji wa kila kitu; lugha na binadamu ni viumbe vyake.

### (ii) Asili ya Lugha na Tofauti ya Ndimi

Mgogoro haukuishia kwenye fasili ya lugha tu bali ulipanuka na kugusia asili ya lugha. Juhudi za kutafuta chanzo cha lugha zilifanyika kwa karne kadha na watu wengi wakiwemo wanaisimu wa kimagharibi. Pamoja na hayo juhudi hizo ziligonga mwamba kwa sababu zilikwepa kwa makusudi kuihusisha asili hiyo na Mwenyezi Mungu. Matokeo yake yalikuwa kutoa maamuzi kwamba pasiwepo utafiti unaojihusisha na asili ya lugha (1989, Crystal). Jambo hilo, limetoa fursa kwa waitifaki wa kidini kudhihirisha mtazamo wao dhidi ya Wasekula wasiotegea sikio mambo yanayomhusu Mwenyezi Mungu. Uislamu hufundisha kuwa mwanadamu ameumbwa na Mwenyezi Mungu ambaye alimjalia lugha ili aitumie katika kuendesha mambo yake duniani. Katika sehemu mbalimbali za Kur'ani, asili ya lugha imegusiwa sambamba na asili ya mwanadamu. Ushahidi wa kuthibitisha kuwa lugha ni neema ambayo Mwenyezi Mungu amemjaalia mwanadamu baada ya kuumbwa kwake ni:

Kwanza, Kur'ani (55:1-4): 'Ar-Rahaman (Mwenye Kurehemu); alifundisha Kur'ani. Alimuumba mwanadamu; Akamfundisha kunena (lugha)'. Huu ni ushahidi kwamba asili ya lugha ni sawa na asili ya mwanadamu. Kwani aliyemuumba ndiye aliyemfunza lugha. Wafasiri wa Kur'ani wanasema maana ya "*Al-bayaan"* katika tamko "*Allamahu Al-bayaan*" ni kutamka ama kunena (An-nutq). Kwa hiyo, mwanadamu aliumbwa kwa namna ambayo inamwezesha kutoa matamko kadha wa kadha. Ndiyo maana ala alizojaaliwa kinywani hurejelewa kama ala za matamshi. Kwani hazimfai tu katika kula na kunywa, bali muhimu zaidi huzitumia katika kunena ambayo ni sifa kuu ya lugha ya mwanadamu.

Pili, Kur'ani (2:30-31), 'Hakika nitamweka katika ardhi khalifa' (Malaika) wakasema: utaweka humo (yule) ambaye atafanya ufisadi ndani yake na amwage damu? Akasema: Hakika mimi najua yale msiyoyajua. Akamfunza Adam majina yote …' Hii ina maana kwamba alimfunza viashiria (*signifiers*) na viashiriwa (*signified*).

Tatu, Kur'ani (90:8-9), 'Je, Hatukumjalia (mwanadamu) macho mawili? na ulimi na midomo miwili?' Hapa Mwenyezi Mungu anatueleza kuwa yeye ndiye anayehusika na maumbile ya mwanadamu na lugha yake. Kwani macho ndiyo yanayotumika katika kuviona vitu halisi (viashiriwa) nayo kajaaliwa mwanadamu; ili asionekane kama bubu mbele ya viashiriwa hivyo, akajaaliwa ala za matamshi za kutumia katika uzalishaji wa sauti zinazotumika katika lugha.

Ulimi na midomo hurejelewa na wanaisimu kama ala sogezi. Kusogea sogea kwake ndiko kuna komwezesha mtu kutamka. Kwa hivyo, aya hiyo hudhihirisha kuwa lugha kama mfumo wa sauti unaotumiwa na watu katika mawasiliano, asili yake ni Mwenyezi Mungu. Kwani kwa mujibu wa aya hiyo, Mwenyezi Mungu ndiye aliyemfundisha mwanadamu lugha na kumpa vyenzo za matamshi, kwa maana ala za matamshi.

Nne, Kur'ani (49:13), Katika sura hii Mwenyezi Mungu anaelezea asili moja ya lugha na mwanadamu licha ya tofauti zao. Anasema: 'Enyi watu! Hakika sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume mmoja (Adamu) na mwanamke mmoja (Hawa), tukakujaalieni mataifa na makabila mbalimbali, ili mjuane (siyo mkejeliane). Hakika aliye mbora kati yenu mbele ya Mwenye Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi'. Aya hii, inaelezea kuwa lugha asili na chanzo chake ni Mwenyezi Mungu. Na inapaswa kutumika kwa utangamano wa kitaifa; na utambulisho wa kijamii na siyo kudharauliana na kubaguana. Kwani lugha si kielelezo cha ubora wa mzungumzaji wake. Uchamungu ndiyo hoja. Uchamungu hufikiwa kupitia juhudi za kushiriki kikamilifu katika vitendo vya ibada; na mwanadamu hakuumbwa isipokuwa kwa ajili ya kumwabudu Mwenyezi Mungu. Hivyo, lugha ya paswa itumike kukidhi matilaba hayo, (Kur'ani, 51:56).

Tano, Kur'ani (30:20-25), 'Na katika dalili zake ni kuhitilafiana kwa ndimi zenu na rangi zenu'. Tofauti ya lugha na lahaja zake ni dalili ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, ukwasi wake na uwezo wake juu ya kila kitu. Tofauti ya rangi za watu ni dalili vivyohivyo.

Kwa hivyo, asili ya lugha ni Mwenyezi Mungu kwa mtazamo wa kidini. Hii ndiyo kusema, ikiwa Mwenyezi Mungu aliweza kumuumba mwanadamu kutokana na udongo, akawaumba watu wote kutokana na Adamu na Hawa; akawaumbia wanaume na wanawake na kuwafanya wenye kutulizana mitima yao, akajalia baina yao upendo na huruma kupitia ndoa (Kur'ani, 30:20-21). Ikiwa aliweza kufanya maajabu hayo yote, basi bila shaka hawezi kushindwa kumfunza mtu lugha kwani akitaka jambo hutokea tu kwa amri ya '*kun fayakun*' yaani, kuwa na likawa. "Hakika amri yake anapotaka jambo ni kusema "kuwa", na likawa (jinsi alivyotaka); basi ametukuka Yule ambaye mikononi mwake kuna mamlaka juu ya kila kitu na kwake ndiko mtarejeshwa". Surat Yasin (36:82).

**(iii) Sifa za Lugha**

**A. Ubainifu**: Hii ni sifa kuu miongoni mwa sifa za lugha, nayo imeelezewa katika Surat Ar-Rahman aya ya nne ambapo baada ya Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu, alimfunza "*Bayan*" ama kubainisha. Ubainifu tungeutoa wapi? Sauti anazotamka mwanadamu ni bainifu kwa sababu zikibadilishana nafasi katika tamko, huzalisha maneno yenye maana tofauti. Kwa mfano sauti /s/, /z/, /sh/, /k/, /m/, /t/, na /d/ huchukuliwa na wanaisimu kama fonimu kwa sababu zinaweza kutumika katika kuunda maneno maalumu. Tazama mifano ifuatayo:

**S**aka, **Z**aka, **S**haka, **K**aka, **M**aka, **T**aka na **D**aka

Ubainifu ulioelezewa katika sura hiyohiyo uko vilevile katika maneno, virai, vishazi, na sentensi. Vipashio hivyo ambavyo ndivyo vikubwa zaidi kuliko fonimu vina maana bainifu. Maana hizo ndizo zinazomwezesha mzungumzaji kuwasilisha fikra na maono yake na kufanikisha mawasiliano baina ya washiriki mbalimbali. Kwa mfano, sentensi zifuatazo ni kamili kwa sababu zimeundwa kutokana na sauti na maneno au virai bainifu:

(i) Askari polisi waliwasaka wahalifu
(ii) Waumini walitoa zaka
(iii) Sitilii shaka uwezo wa Mwenyezi Mungu
(iv) Kaka yake alienda Saudia
(v) Nirejeshee mkoba wangu! Mama yake alimaka
(vi) Alitupa takataka kwenye jaa la taka

(Byakutaga, 2000).

**B. Upangilifu**: Sifa hii hudhihirika katika uundaji wa maneno na sentensi. Mwanadamu hufuata mfano maalum ambao kajaaliwa na muumba wake katika uundaji wa maneno. Maneno hayaundwi kiholela. Vivyohivyo, virai, vishazi na sentensi haziundwi kiholela. Kuna mpangilio maalumu ambao wanadamu hufuata ulioko ubongoni. Mwenyezi Mungu kamjalia mwanadamu kipawa cha kuzingatia mpangilio unaokubalika na jamii lugha anapounda maneno wakati wa mawasiliano. Hebu tuangalie mifano ya mpangilio katika lugha zifuatazo:

(i) Kiwango cha Maneno:

| Mpangilio Faafu | Mpangilio Usiofaa |
|---|---|
| Kalamu | Mulaka |
| Kitabu | Butaki |
| Shule | Leshu |
| Mwallimu | Mulimwa |
| Mwanafunzi | Nzifunamwa |

(ii) Kiwango cha Sentensi

| Mpangilio Faafu | Mpangilio Usiofaa |
|---|---|
| Mimi ni mwalimu | Ni mwalimu mimi |
| Mtoto hodari amefaulu mtihani | Hodari mtoto mtihani amefaulu |
| Haba na haba hujaza kibaba | Kibaba hujaza haba na haba |

**C. Ubunifu:** Mwanadamu amejaaliwa na Muumba wake sifa nyingine ambazo ni muhimu sana. Sifa hizi humwezesha kubuni na kutamka maneno mapya ambayo hajawahi kufikiria juu yake. Mwenyezi Mungu ndiye anayemwezesha kufanya hivyo kwani katuambia Mwenyewe kwamba alimfanya mwanadamu 'Albayana' yaani kujieleza, kuelezea mambo kadhaa, kunena ama kutamka. Ubunifu hupatikana takribani katika sifa zote za lugha.

**D. Ubobeaji**: Hii ni mojawapo ya sifa wanazozitaja wanaisimu kuwa ni upekee wa lugha ya mwanadamu. Wanahoji kuwa, tofauti na wanyama, mwanadamu huendelea kuchapa kazi yake huku akiongea bila shida yoyote. Hana haja ya kusitisha kazi kwa minajili ya kuongea na mtu mwingine. Anaweza kulima, kuandika, kuendesha gari, kujenga nyumba, kutembea ilhali anazungumza, bila tashwishi yoyote, tofauti na viumbe wengine. Inasemekana kuwa nyuki anapotoa taarifa kuhusu maeneo yenye maua, hucheza tu densi. Hafanyi kazi nyingine. Sifa hiyo hudhihirisha kuwa maumbile ya mwanadamu ni tofauti na yale ya viumbe wengine; ndiyo maana hata lugha yake ikawa tofauti na ile ya viumbe hao. Mwenyezi Mungu anasema:

"Ewe mwanadamu! Ni nini kilichokughuri ukamwacha Mola wako mlezi mtukufu. Aliyekuumba na akakuweka sawa, akakunyoosha. Katika kila sura yoyote aliyopenda akakujenga", (Al-infitwar: 6-8). Kuwepo kwa sifa hiyo katika maumbile ya mwanadamu

ni kielelezo cha uwezo wa Mwenyezi Mungu juu ya kila kitu na ni dalili kwamba yeye ni hodari katika uumbaji wake.

**E.** **Urithishaji**: Wanaisimu wa kimagharibi hukiri kwamba mwanadamu harithishwi lugha kama anavyomrithi mzazi wake mambo mengine. Ndiyo maana ukamkuta mtoto wa Kihindi akikulia katika mazingira ya Kichina, lugha anayoipata ni ya Kichina na siyo Kihindi hata kama umbile lake ni la Kihindi, (Byakutaga, 2000). Mwenyezi Mungu ndiye anayemjaalia uwezo wa upataji wa lugha hiyo badala ya lugha mama, kwani humfundisha mtu asiyoyajua (Al-Alaq: 1- 4).

**F.** **Uwili**: Sifa hii haitofautiani sana na ile ya ubainifu. Ijulikane kwamba Mwenyezi Mungu alimjaalia mwanadamu viungo mahsusi kwa ajili ya kutamkia. Viungo hivi hujulikana kitaaluma kama ala za matamshi; ala hizo ni midomo, meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini, umio, kanda sauti, glota, ulimi, mapafu, na pua. Ala hizo huhusika kwa namna moja au nyingine katika kuzalisha sauti mbalimbali. Wakati wa kutamka, mwanadamu hufanya mambo mawili:

Kwanza, hutoa sauti bainifu amabayo hutumika kuundia maneno mbalimbali. Pili, maneno yanayoundwa huwa na maana bainifu. Hivyo basi, mchakato wa kuzalisha sauti na maneno yenye maana bainifu humwezesha mzungumzaji kuendesha shughuli ya kuwasiliana na wenzake. Sauti za wanyama haziwezi kuchanganuliwa kwa namna hiyo kwa sababu viungo vyake havikupewa jukumu linguine isipokuwa kula na kupumua. Kiumbe aliyepangiwa jukumu la ukhalifa ni mwanadamu peke yake “Hakika mimi nitamweka katika ardhi khalifa[2] …”, (Kur’ani, 2:30). Aidha mwanadamu ndiye aliyetwishwa mzigo wa kumuabudu Mwenyezi Mungu kama anavyosema: “Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu”, (Kur’ani, 51:56).

**(iv) Ujuzi wa Lugha**

Kama tulivyokwisha taja, Mwenyezi Mungu ndiye aliyemfunza mwanadamu lugha ikiwa ni miongoni mwa mambo mengi ambayo alikuwa hayajui. Mwenyezi Mungu anasema: “Amemfundisha mwanadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui”, (Kur’ani, 96:5). Mtu

[2] Mfwatizi

aliye na sifa tulizopitia hapo awali huwa na ujuzi wa lugha. Mjua lugha sharti awe anazijua sauti zote za lugha husika (fonimu na alofoni zake), maneno (mofimu na alomofu zake), awe na umilisi wa kisarufi na kimawasiliano unaomwezesha kutunga sentensi zinazokubalika na jamii lugha. Hali hii humwezesha kuwa na ufasaha wa lugha ambao ndio kiungo muhimu katika ujuzi wa lugha, (Wardhaugh, 2006: 2-3).

**(v) Dhima ya Lugha**

Lugha ni chombo muhimu katika maisha ya mwanadamu. Maisha bila ya lugha hayawezi kutabirika. Hakuna shughuli inayoendeshwa pasi na kuihusisha lugha. Lugha ni muhimu katika maisha ya mwanadamu kama ulivyo ulimi katika mwili wa mwanadamu. Hutumika kama kitambulisho cha binadamu na jamii yake, chombo cha kufikiria, mawasiliano, kufundishia, kutekelezea ibada, na kutendea kazi mbalimbali:

Kwanza, lugha hutekeleza dhima ya kumtambulisha binadamu pamoja na jamii yake. Mwili wa mwanadamu umejaaliwa viungo sawa na vile walivyojaaliwa wanyama. Ndiyo maana anarejelewa wakati mwingine kama mnyama. Pamoja na hayo amejaaliwa tunu inayomfanya kuwa bora kuliko mnyama wa kawaida. Tunu hii humuinulia hadhi na kumtoa kwenye uhayawani hadi kwenye daraja la ubinadamu. “Bila shaka yumemuumba mwanadamu kwa umbo lililo bora kabisa”, (Kur’ani, 95:4 na 82:6–7).

Ubinadamu wa mwanadamu hautambuliki kwa jambo jingine isipokuwa kwa tunu hiyo ambayo ni lugha. Mtu hutambulika kwa urahisi sana kutokana na lugha anayozungumza. Mswahili atatambulika kwa Kiswahili chake. Vivyo hivyo Mwarabu, Mzungu, Mjapani na Mchina watatambulika kwa lugha zao ambazo ni Kiarabu, Kijapani na Kichina. Lugha anayozungumza ndiyo huitambulisha jamii anayotoka kwani hakuna jamii isiyokuwa na lugha na hakuna lugha isiyojikita katika jamii. Uislamu umeelezea dhima hiyo katika Kur’ani (49:13).

Pili, lugha hutekeleza dhima ya kufikiria mambo makuu yanayotarajiwa kufanyika, hutimia kwa kufikiria kwanza kisha ndiyo utekelezaji. Huo mchakato wa kufikiria, hauwezi kuwepo bila ya lugha. Fikra huibuka na kuibuliwa kwa kutumia lugha maalumu. Fikra hizo huandikwa kwenye karatasi halafu zikawekwa vitendoni katika muda mwafaka.

Tatu, kama si lugha mawasiliano baina ya watu yangekuwa magumu. Ingawa kuna njia nyengine za mawasiliano lakini watu huwasiliana kwa wepesi baina yao wanapoendesha shughuli za kibiashara, kisiasa, kidini na kijamii kwa kutumia lugha.

Nne, lugha hutekeleza dhima ya kusambaza elimu na maarifa. Mtume (S.A.W) alisema: Mwenyezi Mungu amemsifia mtu anayesikia maneno yangu kisha akayasambaza. Hivyo, kulingania ni sehemu moja miongoni mwa njia za kutoa elimu. Ulinganizi kwa kawaida hutoa elimu na mafundisho ya kiimani, kwa muktadha wa makala hii ni kulingania Uislamu kupitia lugha.

Tano, lugha husambaza tamaduni za jamii mbalimbali kupitia kazi za fasihi. Utamaduni wa Kiislamu uliweza kuwafikia Waislamu kupitia Kur’ani tukufu na hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W). Ujumbe uliomo kwenye vitabu hivyo husomewa Waislamu misikitini na katika sherehe mbalimbali kama vile sherehe za harusi, maulidi, akika na katika hotuba za Ijumaa na Iddi. Lugha ya Kiarabu ndiyo hutumika sambamba na lugha za Kienyeji. Hivyo, Kur’ani na hadithi za Mtume (S.A.W) huchukua nafasi ya kazi za fasihi katika jamii za Waislamu katika kusambaza utamaduni.

Sita, lugha hutekeleza dhima ya kuelezea maana fiche, kutoa ufafanuzi wa matamko kadha wa kadha na vilevile kutafsiri vitabu na kutoa huduma ya ukalimani. Kutokana na dhima hii wataalamu mbalimbali wa Kiislamu walihimiza ufundishaji wa sarufi ya Kiarabu. Miongoni mwa wataalamu hao ni Alkhalil Ahmed, Sibawaih na Ibin Taimiyah. Hapa ieleweke kuwa lugha ya Kiarabu ndiyo iliyoshushiwa mafundisho ya Uislamu. Ili muumini ayafahamu vyema mafundisho ya dini yake hana budi kujifunza Kiarabu. Elimu ya tafsiri nayo imeyahawilisha mafundisho hayo kuelekea katika lugha za kienyeji.

Saba, lugha hutumika kama hifadhi ya elimu na maarifa ya kidini na kidunia. Elimu ya Kiislamu, kwa mfano, imehifadhiwa katika lugha ya Kiarabu iliyotumika kuandikia Kur’ani Tukufu, hadithi za Mtume (S.A.W) na vitabu vya madhehebu mbalimbali na taaluma kadha wa kadha.

Nane, lugha hutekeleza dhima ya kufanikisha ibada. Kwa mfano, hakuna namna ambayo Shahada, Sala na Hija zinaweza kufanyika pasi na kutumia lugha. Anaye silimu hulazimika kutamka shahada, anaye sali huanza kwa kuadhini kisha akasoma Kur’ani na adhkari kadha wa kadha. Vitendo vya Hija hufanywa kwa kutamka nia ya kuhiji na kuendelea kumhimidi na

kumsifu Mwenyezi Mungu pamoja na kusali. Lugha inayotumika katika vitendo hivyo vyote ni Kiarabu. Mwisho kitendo cha ndoa kinachoanza kwa kutafuta mchumba maneno ya kuraiana ili waoane, kupeleka posa na kumalizika kwa kufunga ndoa, huhusisha lugha pa kubwa. Ushawishi wa hali ya juu huhitajika katika mchakato mzima wa kufunga ndoa; lugha ndiyo hutumika kukidhi matlaba hayo. Katika kufunga ndoa kuna kupokezana kwa matamko maalumu; huku mwenye mamlaka juu ya msichana akisema ‘Nakuozesha binti yangu fulani kwa mahari kadha kulingana na mafundisho ya Kur’ani na Sunna za Mtume Muhammad (S.A.W). Je, Umekubali?’. Anayeoa hushurutishwa kujibu kauli hiyo kwa kusema ‘Nimekubali kumuoa fulani binti fulani …”, (Brow na Yule).

**vi) Lugha Bora na Shenzi**

Kuna wanaoshikilia mtazamo kwamba baadhi ya lugha kwamba ni bora kuliko nyingine Mtazamo huu umejengwa kwa misingi ya kibaguzi. Syeed, (1984) anasema Uislamu hushikilia kwamba watu wote ni sawa. Hakuna tofauti kati yao japokuwa wanatofautiana katika rangi, makabila na mataifa yao. Surat Al Hujrat inaelezea mambo hayo kinagaubaga. Mwenyezi Mungu anasema: ‘Enyi watu! kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adamu)’na (yuleyule) mwanamke (mmoja; Hawa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane (tu basi, siyo mkejeliane). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni mjuzi zaidi, mwenye habari (za mambo yote), (Kur’ani, 49:13).

Kama tulivyoona hapo awali hakuna jamii isiyokuwa na lugha na hakuna lugha isiyojikita katika jamii. Unapozungumzia lugha huwa unazungumzia jamii fulani. Ndiyo maana kisawe cha lugha kikawa ni ulimi na ndimi huwa nazo watu, wanazozitumia kama ala muhimu katika utamkaji. Tunawasikia mara nyingi watu wakisema: ‘lisanul Arab’ au ‘mother tongue’ au ‘olulimi oluswayili’ wakimaanisha ‘lugha ya Kiarabu, lugha mama na lugha ya Kiswahili’. Lugha hufungamanishwa na jamii ya wazungumzaji wake. Kwa hivyo, Lugha ya Kiarabu ni lugha inayozungumzwa na watu wa jamii ya Kiarabu, lugha ya Kizulu huzungumzwa na watu wa jamii ya Wazulu na lugha ya Kichina inazungumzwa na Wachina.

Ni wazi kwamba kuzinyanyulia hadhi baadhi ya lugha na kuzidunisha nyingine huashiria hali ya kuzibagua jamii. Ikiwa mwelekeo wa kuwabagua watu unakataliwa katika Uislamu, basi ni dhahiri kwamba kuibagua lugha kumekatazwa pia. Watu wote ni sawa mbele ya Mwenyezi Mungu kama ambavyo lugha zilivyo sawa. Mtume Muhammad (S.A.W) alisema: "Nyote ni sawa kama meno ya kitana. Hakuna tofauti baina ya mtu mweupe na mweusi isipokuwa katika uchamungu"; akimaanisha kwamba hakuna ubora wa Mwarabu juu ya Mwajemi isipokuwa katika uchamungu.

Kwa mujibu wa Al – Munjid, kamusi ya Kiarabu (1998), Mwajemi ni Mfursi au mtu yeyote asiyetokana na jamii ya Waarabu. Ni wazi kuwa watu wote ni sawa, hakuna jamii iliyo bora kuliko nyingine. Darubini ya Kiislamu humuona mchamungu kuwa ndiye bora hata kama rangi yake haipendezi katika mboni za watu wengine kama wadhaniavyo.

Kimantiki na kisayansi hoja inayokubalika ni ile isiyozingatia hisia za mtu. Bali huzingatia ukweli na kuepukana na upendeleo. Wanaochukulia lugha za wenzao kuwa ni lugha shenzi hupendelea lugha zao. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi wa kila kitu na ana habari juu ya mambo yote ambayo binadamu hayajui. Hivyo, anachotuambia Mwenyezi Mungu ni kwamba watu wote ni sawa licha ya lugha, rangi, mataifa na makabila yao.

Ikumbukwe kwamba, wanaisimu wanakiri kuwa ingawa lugha zinatofautiana, kimsingi zina sifa bia. Kwanza, zote zina vokali na konsonanti na maneno yake hundwa kwa kuunganisha silabi kadhaa; na pili zina maneno toshelezi yanayowakilisha dhana mbalimbali, (TByakutaga, 2000 Greenberg, 1966 na Masamba, 1996).

**vii) Lugha ya Mwanzo**

Kinachokusudiwa hapa ni lugha ya mwanadamu na siyo jambo jingine; hii ni kwa sababu kwa mtazamo wa kiimani lugha kwa ujumla wake imekuwa ikitumika katika mawasiliano baina ya Mwenyezi Mungu na viumbe wake alivyoviumba mwanzo - kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu. Kur'ani inaeleza kuwa lugha ya mwanadamu - Mwenyezi Mungu ndiye aliyemfundisha mja wake Adamu ambaye ndiye baba wa kwanza wa watu wote, ndiyo maana wanaitwa wana-Adamu, yaani watoto wa Adamu.

Mwenyezi Mungu alimuumba Adamu (A.S) kisha akamfunza lugha. Kwa vile, kumekuwa na utashi wa kutaka kujua ni lugha gani iliyozungumzwa mwanzo, kwa mtazamo wa Kiislamu lugha ya mwandamu ilifunzwa kwa mwanadamu wa kwanza mara tu baada ya kuumbwa kwake. Katika surat Al Baqara, Mwenyezi Mungu anasisistiza jambo hilo na kutoa taarifa ya ziada kwa kusema:

"Na tulisema (baada ya hapo kumwambia nabii Adam): Ewe Adam kaa wewe na mkeo katika bustani hii (peponi); na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini msiukaribie mti huo tu; msije kuwa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao kwa kukhalifu amri za Mwenyezi Mungu), (Kur'ani, 2:35 na 7:19). Lakini Iblis alitumia lugha ya ushawishi kuwatelezesha na wakakhalifu amri ya Mwenyezi Mungu. Yaani, aliwarai waikhalifu amri ile, hatimaye wakala katika mti huo waliokatazwa na akawatoa katika (hali) waliyo kuwa nayo. Tukawaambia: nendeni hali ya kuwa maadui nyinyi kwa nyinyi, na makazi yenu (sasa) katika ardhi, na mtapata starehe humo kwa muda (mahsusi), (Kur'ani, 2:36).

Pia, Kur'ani (2:20 na 7:21) imeelezea ushawishi huo wa shetani kwa kusema: "Basi shetani; (naye ni yule Ibilisi), aliwatia wasiwasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa, na akasema: 'Mola wenu hakukukatazeni mti huo ila msije kuwa malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele (wasife)' Ili kuwatia hamu zaidi ilibidi awaapie "naye akawaapia (kuwaambia), kwa yakini mimi ni mmoja wa watoao shauri njema kwenu".

Hapa Iblisi anazungumza na Adam na Hawa ili waridhie ushawishi wake na anatumia mbinu ya kuapa ili wasimtilie wasiwasi katika madai yake. Adamu na Hawa walielewa lugha hiyo wakaitikia matakwa ya Iblisi pasi na kujua kwamba anakusudia kuwaangamiza. Walipotambua kosa lao walitubia juu ya dhambi zao kwa kutumia maneno waliyoyapokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu. "Wakasema: Mola wetu tumedhulumu nafsi zetu na kama hutatusamehe na kuturehemu bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara (kubwa kabisa)". Kwa hiyo lugha ilizungumzwa mwanzo bustanini baina ya Mwenyezi Mungu, Malaika, Adam na mkewe. Kihebrania hakiwezi kuwa lugha ya kwanza kama wanavyodai wanaodai kwa sababu Adamu na Hawa hawakuwa Wahebrania.

Kutokana na kitendo hicho cha kumuasi Mwenyezi Mungu, Adamu na mkewe walifurushwa peponi wakaja kuishi ardhini kama tunavyoambiwa katika Kur'ani, (7:24-25) kuwa "Akasema

(Mwenyezi Mungu). Shukeni (katika ardhi), nyinyi kwa nyinyi ni maadui. Na makao yenu yatakuwa katika ardhi; na starehe yenu pia; mpaka muda (niutakao mimi Mwenyezi Mungu). Akasema: (Mwenyezi Mungu): Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo' (na mtafufuliwa kwenda Akhera kulipwa)".

Kwa hivyo mwanadamu alijaaliwa lugha tangu alipoumbwa na kuwekwa bustanini akawa wanawasiliana kwayo na Muumba wake. Baada ya kuumbiwa mke wake aliendelea kuitumia katika mazungumzo yao ya kila siku hadi pale shetani alipowashawi kumuasi Muumba wao. Walipofukuzwa mbinguni waliishi katika ardhi wakazaliana wakawa bado wanaitumia lugha hiyo kwa manufaa yao na vizazi vyao kwa ujumla.

Baada ya kubaini mahali lugha ya binadamu ilipozungumzwa mwanzo, suala la kujiuliza ni je, lugha hiyo iliitwaje? Jibu la swali hilo ni gumu kwa sababu hatukuambiwa na Mwenyezi Mungu kupitia mafundisho ya Uislamu. Tunachoweza kusisitiza hapa ni kwamba kwa vile Adamu ndiye kiumbe wa kwanza katika jamii ya watu aliyefunzwa lugha, basi lugha hiyo inaweza kupewa jina la 'lugha ya Adamu'. Hii ni kwa sababu lugha hupewa majina ya watu wanayoizungumza au jamii inayoitumia. Jamii ya kwanza ilikuwa jamii finyu kabisa kwani iliundwa kwa Adamu na mkewe Hawa. Baada ya kuzaliana, jamii yao ilipanuka ndiyo baadaye pakapatikana jamii lugha pana. Jamii hizi ziliendelea kukuwa na kusambaa pakazuka lahaja na lugha mbalimbali. Kutokana na hali hiyo, Mwenyezi Mungu aliwatumia watu mitume kuwabainishia mafundisho yake kwa lugha hizo mbalimbali. Kama Kur'ani isemavyo: "Na hatukumpeleka Mtume yoyote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili apate kuwabainishia. Kisha Mwenyezi Mungu anamwacha kupotea amtakaye (kwa kuwa mwenyewe hataki kuongoka); na humuongoza amtakaye. Naye ni mwenye nguvu na mwenye hikima, (Kur'ani, 14:4). Aya hizo zinadhihirisha kwamba tangu jadi kumekuwepo jamii lugha anuai na kila jamii lugha imewahi kutumiwa mtume. Mathalan, katika Surat Al Aaraf tunapata baadhi ya kaumu zilizotumiwa mitume:

A. Kaumu ya Nuhu (AS). Tulimpeleka Nuhu kwa watu wake, naye akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu (mwingine) ila yeye. Hakika mimi nakuhofieni adhabu ya siku (hiyo) iliyo kuu, (Kur'ani, 7:59). Watu wake walimjibu: '… sisi tunakuona umo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri (kwa kutukataza haya tuliyowakuta nayo wazee wetu Akasema: Enyi Kaumu yangu! mimi simo katika upotofu) lakini mimi ni mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu wote, (7:60-64).

B. Kaumu ya Adi. “Na kwa Adi (tulimpeleka) ndugu yao Hud...”, (7:65-72).
C. Kaumu ya Thamud (AS). “Na kwa Thamud (tulimpeleka) ndugu yao Saleh …”(7:73-78).
D. Kaumu ya Lut (AS). “Na (tulimpeleka) Lut: Basi (wakumbushe watu wako) alipowaambia kaumu yake: Je, mnafanya jambo chafu ambalo hajakutangulieni yoyote kwa (jambo chafu hilo katika ulimwengu!...)”, (7:80-84).
E. Kaumu ya Shuaib (AS). “Na kwa watu wa Madayan (tulimpeleka) ndugu yao Shaibu, akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu”, (7:85-93).
F. Kaumu ya Musa. “Kisha baada ya (mitume hao) tukampeleka Musa na hoja zetu kwa Firauni na watu wake. Lakini wakazikataa. Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu”, (7:103-156).
G. Umma wa Muhammad (S.A.W). “Ambao wanafuata Mtume, Nabii aliye Ummy (asiyejua kusoma wala kuandika, na juu ya hivi atafundisha mafundisho hayo ya ajabu ya Uislamu), ambaye wanamuona ameandikwa kwao katika Taurati na Injili; ambaye anawaamrisha mema na anawakataza yaliyo mabaya na kuawahalalishia vizuri na kuwaharamishia vibaya, na kuwatolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao (yaani sharia ngumu za zamani mila za kikafiri). Basi wale waliomuamini yeye na kumuheshimu na kumsaidia na kuifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye (yaani Qur’an) hao ndio wenye kufaulu”, (7:157).

Ushahidi huo unathibitisha kwamba baada ya lugha ya Adamu, lugha nyingine zilizuka kutokana na kuzaliana, kusambaa na kutengana kwa watu. Lugha hizo ni za jamii mbalimbali na zinaweza kuitwa lugha za mataifa. Kwa maana, mitume mbalimbali walitumwa kwa kaumu zao kwa ajili ya kuwafundisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa kutumia lugha zao.

Mtume aliyetajwa mwisho alitumia Kiarabu japokuwa alitumwa kwa watu wote kama tunavyoambiwa katika surat Al Aaraf (7:158). “Sema (Ewe Nabii Muhammad) ‘Enye watu!’ Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote …”, Hii ni kwa sababu alikuwa Mwarabu na waumini wake wa mwanzo kabisa walikuwa Waarabu na Kur’an tukufu imeshushwa kwa lugha hiyo. Fauka ya hayo, ibada za Uislamu kama vile Sala na Hija hufanywa kwa Kiarabu hata kama muumini si Mwarabu ili kudumisha utangamano wa umma wa Kiislamu unaotokana na jamii mbalimbali.

## Hitimisho

Kwa kurejelea mtazamo wa imani ya Kiislamu, inabainika wazi kwamba chanzo cha lugha ni Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye aliyemjaalia mwanadamu lugha ili aweze kuutawala ulimwengu kwa niaba yake. Kupitia mawasiliano yao (wanadamu) waweze kuishi kama Mwenyezi Mungu alivyowataka waishi katika ulimwengu huu. Wanadamu wanapaswa kutambua kwamba lugha ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu (Kur'ani,102:8). Hivyo, wanadamu hawana budi kuitumia lugha ipasavyo huku wakiamini kwamba kuna siku wataulizwa jinsi walivyoitumia katika maisha yao ya kila siku kwa muda wao wote wa uhai wao hapa duniani.

## Marejeleo


Brown, G. and Yule, G. (1988). Discourse Analysis. Cambridge: Cambridge University Press.

Byakutaga, S. C. (2000). An introduction to the Study of Language. Kampala: the New vision Printing and Publishing Corporation.

Crystal, D. (1986). What is Linguistics. Victoria: Edward Arnord.

Fromkin, V. and Rodman, R. (1993). An introduction to Language. Harcourt: Brace Jovanovich

Greenberg, J.H. (1966). Language Universals. The Hague: Mouton.

Massamba, D. (1996). Phonological Theory. Dar es Salaam

Mgullu, R.S. (2012). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia. Nairobi: Longhorn Publishers

Nkwera, F. (1978) Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Tanzania

Syeed, S. M. (1984). Islamization of Linguistics. In: Towards Islamization of Disciplines. Kwalalumpar: International Institute of Islamic Thought.

Wardhaugh, R. (2006). An Introduction to Sociolinguistics (Fith Edition). Victoria: Blackwell Publishing Limited.